



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA

## TANGAZO LA UZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma anawatangazia wananchi wote, taasisi za umma na taasisi binafsi kuwa Halmashauri imepima viwanja vya matumizi mbalimbali katika eneo la Makao makuu ya Halmashauri Suguti Kwikonero.

Viwanja vinapatikana nyuma ya HOSPITALI YA HALMASHAURI KWIKONERO kuangalia Ziwani mkabala na Makao makuu ya HALMASHAURI. Umeme unapatikana katika eneo vilipo viwanja na barabara zimefunguliwa na kuchongwa ili kurahisisha kufikika kwa kila kiwanja. Viwanja hivi vitauzwa kuanzia tarehe 20/11/2022 hadi tarehe 20/02/2023.

Wananchi wote wenye kuhitaji viwanja wafike katika Ofisi ya Ardhi au Uhasibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma iliyopo Gineri Nyang'oma- Mugango au Musoma mjini mkabala na Uwanja wa ndege Musoma kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi ya kiwanja. Fomu itagharimu shilingi 20,000/=(isiyorejeshwa) ambayo italipwa kwa namba ya malipo (Control Number) atakayopatiwa mteja.

Mnunuzi ataswa kukamilisha malipo ya kiwanja ndani ya miezi miwili (siku 90) tangu tarehe ya kupewa ankara ya gharama za ununuzi wa kiwanja ambapo watakaoshindwa kukamilisha malipo, viwanja walivyogawiwa vitatangazwa upya na kugawiwa kwa wateja wengine.

### Bei za Viwanja

| Na | Matumizi ya Ardhi  | Bei kwa mita ya Mraba |
|----|--------------------|-----------------------|
| 1. | Makazi             | 1000                  |
| 2. | Makazi na biashara | 1000                  |
| 3. | Biashara           | 1200                  |
| 4. | Maeneo ya kuabudia | 1500                  |

Tangazo hili limetolewa na :

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA